Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 -9289]



Issue no: 01 | **Vol no:** 07 | **September** 2026: 122-136

Uainishaji wa Vishazi Tegemezi Katika Sentensi za Kibukusu

Shadrack Kulabusia [(1)]
Harrison Ogutu [(2)]
Rose Masai Mavisi [(3)]

(1.2.3) Catholic University of Eastern Africa, Kenya.
Main author's email: kulabusias@gmail.com

Article History
Received: **2026.07.13**
Accepted: **2026.08.15**
Published: **2026.09.12**

Cite this article in APA
Kulabusia, S., Ogutu, H., & Mavisi, R. M. (2026). Uainishaji wa vishazi tegemezi katika sentensi za Kibukusu. *Editon consortium journal of Kiswahili, 7*(1), 122-136. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.771

Ikisiri
Makala hii ilichanganua aina za vishazi tegemezi katika sentensi za Kibukusu, lahaja kubwa ya jamii za Kiluhya inayozungumzwa Magharibi mwa Kenya. Licha ya tafiti nyingi kuhusu fonolojia na mofolojia ya Kibukusu, sintaksia yake, hasa vishazi tegemezi, haijapewa umakini wa kutosha. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya X-Baa kubainisha aina za vishazi tegemezi vinavyotumika katika mawasiliano ya wazawa wa Kibukusu. Data zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa 15, wakiwemo wanafunzi 7, walimu 5 wa Kiswahili na wazee 3, katika Gatuzi Dogo la Sirisia, Kaunti ya Bungoma. Usampulishaji wa kimakusudi na mpokezano ulitumika, huku data zikikusanywa kupitia uchunzaji mahuluti, mahojiano ya kina na midahalo ya vikundi lengwa. Data zilizorekodiwa zilinakiliwa na kuchanganuliwa kimaelezo, na kuzalisha tungo 129. Matokeo yalibainisha aina sita za vishazi tegemezi: kirejeshi, cha mahali, cha wakati, cha sababu, cha masharti, na kishazi cha utangulizi kinachotumia kiambishi *nekhanja/nekharakikha*. Kishazi hiki cha utangulizi hakijabainishwa katika tafiti za awali za Kibukusu wala katika taipolojia pana ya vishazi tegemezi vya Kibantu. Matokeo yanaunga mkono nafasi ya kishazi kirejeshi kama aina muhimu katika lugha za Kibantu, huku yakipanua mfumo wa kawaida wa aina tatu kwa kuonesha mgawanyiko wa vishazi vielezi katika aina nne na kubainisha aina mpya ya kishazi cha utangulizi. Utafiti unachangia data mpya katika sintaksia ya lugha za Kiafrika na kutoa msingi wa kuhifadhi Kibukusu.

Maneno Muhimu: Kibukusu, sintaksia, uainishaji, vishazi tegemezi, X-Baa.

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Ingawa Kibukusu ni mojawapo ya lahaja kumi na nane za Kiluhya na yenye jamii kubwa zaidi ndani ya kikundi hicho (Sikuku, 2011). Kibukusu kina wazungumzaji wapatao milioni 1.4 katika kaunti za Bungoma, Busia, Trans-Nzoia, na Kakamega. Sintaksia yake, hasa eneo la vishazi tegemezi, imesalia bila kuchunguzwa kwa kina. Hili si tatizo la Kibukusu peke yake, bali ni sehemu ya pengo kubwa zaidi. Licha ya Kibantu kuwa tawi kubwa la familia ya Niger-Kongo linalozungumzwa na watu zaidi ya milioni 350 (Downing na Marten, 2019), lugha nyingi ndogo za Kibantu bado hazijafanyiwa utafiti wa kutosha. Hali hii inasababisha uwakilishi hafifu wa ushahidi wa Kiafrika katika nadharia za kisintaksia zenye uwakilishi wa kimataifa (Paolillo na Das, 2006; Maddieson na Sands, 2019).

Vishazi tegemezi ni vipashio vya kisintaksia visivyoweza kusimama peke yake kama sentensi kamili. Huongeza taarifa ya ziada katika sentensi changamano na kubainisha uhusiano wa kimaana kati ya matukio mawili au zaidi (Massamba, 2004). Kabla ya kuchambua muundo wake wa kina na sheria zinazouongoza, ni muhimu kwanza kubainisha ni aina zipi za vishazi tegemezi zilizopo katika lugha husika. Uchanganuzi wa aina hizo, katika makala hii, unaongozwa na Nadharia ya X-Baa. Mfumo wa kisarufi-zalishi unaoeleza jinsi kila kirai, na hivyo kila kishazi tegemezi, kinavyojengwa karibu na kichwa chake cha kisintaksia (Chomsky, 2020; Radford, 1997). Mfumo huu utafafanuliwa kwa kina zaidi katika sehemu ya “Misingi ya Nadharia” baadaye.

Tafiti zilizopo za Kibukusu zimeangazia maeneo mengine. Mutonyi (2000) alichambua fonolojia, mofolojia, na leksikografia ya lugha hii. Aligusia pia uhusiano kati ya muundo wa vitenzi na uundaji wa vishazi tegemezi. Hata hivyo, hakutoa uainishaji wa aina za vishazi hivyo. Kisembe (2018) alichunguza sheria za uinuaji wa vitenzi na harakati za *wh-* ndani ya vishazi vilivyopachikwa. Alilinganisha sheria hizo na za Kingereza kwa kutumia Nadharia ya Uminimalisti. Utafiti wake haukushughulikia aina za vishazi tegemezi vya vielezi wala miundo yake ya kisarufi. Watulo (2020) alichunguza mfumo wa kipengele cha kitenzi timilifu, utimilifu, mazoea, ukweli, na endelevu na jinsi unavyoathiri uwasilishaji wa taarifa za wakati. Utafiti wake haukubainisha sheria zinazotawala miundo ya vishazi tegemezi. Baligira (2025) anathibitisha kuwa pengo la utafiti wa kisintaksia bado ni kubwa, licha ya wingi wa wazungumzaji wa Kibukusu.Tafiti hizi kwa pamoja zinaonesha mwelekeo mmoja. Mkazo mkubwa umewekwa kwenye fonolojia, mofolojia, na baadhi ya sheria za kisarufi za kitenzi. Eneo la muundo, uainishaji, na utendakazi wa vishazi tegemezi bado halijachunguzwa kwa kina. Hili ndilo pengo la kiusomi linalozibwa na utafiti huu. Kwa kujibu swali: Kuna aina zipi za vishazi tegemezi katika sentensi za Kibukusu?

MAPITIO YA MAANDISHI

Katika isimu hasa kiwango cha kisintaksia, kishazi tegemezi ni sehemu ya sentensi iliyobebwa ndani ya sentensi kuu na haiwezi kujisimamia kimaana. Tafiti nyingi za kitaalamu zimejaribu kudadavua aina za vishazi tegemezi katika sentensi changamano. Hata hivyo, tafiti hizi zimefanywa katika miktadha tofautitofauti kwa kujiegemeza katika nadharia mbalimbali.

Candrasius (2024) alichunguza vishazi tegemezi katika sentensi changamano zilizotokana na tovuti ya habari ya CNN. Kusudi lake kuu lilikuwa kubainisha aina za vishazi tegemezi vinavyotumika katika Kingereza cha kila siku. Matokeo yalibainisha aina tatu kuu: vishazi vya wakati asilimia 55.55, vishazi vya sababu asilimia 22.22, na vishazi vya masharti asilimia 16.66. Vishazi vya wakati vilionekana kutawala. Utafiti wa Candrasius ulitofautiana na utafiti huu. Ulijikita katika Kiingereza ambayo ni lugha ya Kizungu yenye muundo tofauti na lugha za Kibantu. Utafiti huu ulichanganua vishazi tegemezi katika Kibukusu yenye sifa zake za kipekee za kimofosintaksia. Hata hivyo, utafiti wa Candrasius ulinufaisha utafiti huu. Ulitoa msingi wa kulinganisha usambazaji wa aina za vishazi tegemezi, hasa kubainisha ni aina zipi zinazotawala katika Kibukusu.

Vogel (2022) alieleza aina mbalimbali za vishazi tegemezi kamilifu katika Lugha ya Jarawara. shabaha yake ilikuwa kubainisha mfumo wa kina wa uainishaji wa vishazi tegemezi. Hujumuisha vishazi vya kati, vishazi vilivyowekwa kando, na vishazi vilivyowekwa baadaye. Matokeo yalibainisha kwamba kategoria ya wakati haipo katika vishazi vingi vikuu. Hata hivyo, vishazi hivyo vinapaswa kutambuliwa kuwa kamilifu. Jambo hili linapinga mtazamo wa kimapokeo unaounganisha ukamilifu na uwepo wa alama za wakati. Utafiti wa Vogel ulitofautiana kiasi na utafiti huu. Ulichunguza lugha ya Jarawara ambayo si ya familia ya Kibantu. Utafiti huu uliangazia Kibukusu yenye mfumo tofauti wa wakati na ukamilifu wa kishazi. Kwa hivyo, utafiti wa Vogel ulinufaisha utafiti huu kwa namna

fulani. Ulitoa mfumo wa kinadharia wa ufungamanishaji wa vishazi ulioweza kutumika katika uchanganuzi wa muundo sawa katika Kibukusu.

Božić (2022) alichunguza viunganishi vya kishazi kielezi katika Kiingereza na Kikroeshia. Aliangalia jinsi viunganishi hivyo vinavyounda vishazi tegemezi na polisemia yake. Madhumuni yake yalikuwa kuchunguza uwezo wa viunganishi fulani kubeba maana nyingi, hasa jinsi viunganishi vya wakati vinavyoweza pia kutumika kuelezea kisababishi. Alitumia data halisi ya korpus. Matokeo yake yalionesha kwamba viunganishi vya kishazi kielezi ni kundi kubwa na changamano zaidi la viunganishi vya kishazi tegemezi. Maana ya kiunganishi fulani hutegemea sana muktadha wa matumizi yake. Utafiti wa Božić ulitofautiana na utafiti huu kwa njia kadhaa. Ulichunguza lugha za Ulaya zenye muundo wa kisintaksia tofauti na ule wa Kibukusu. Utafiti huu ulizingatia viunganishi vya Kibukusu katika muktadha wake wa asili. Mwisho, utafiti wa Božić uliboresha utafiti huu. Ulitoa mbinu ya kutumia data halisi ya lugha katika kubainisha aina za vishazi tegemezi vilivyotokea kiholela.

Aboh na Essegbey (2010) walionesha muundo wa kishazi katika lugha za Kikwa. Waliangalia muundo wa hoja, mfuatano wa vitenzi, na nafasi ya kitenzi kuhusiana na viashiria vya mtindo. Sababu yao ilikuwa kuelewa jinsi vishazi tegemezi vinavyojengwa katika lugha za Kiafrika. Matokeo yalibainisha kwamba muundo wa kishazi katika lugha hizi una sifa maalum zilizotofautiana na lugha za Ulaya. Hali hii ilihitaji mtazamo wa kipekee wa kitaalamu katika uchambuzi wa lugha za Kibantu. Utafiti huu ulitofautiana na kazi ya Aboh na Essegbey. Wao walichunguza lugha za Kikwa za Afrika Magharibi zenye muundo tofauti na lugha za Kibantu za Afrika Mashariki. Utafiti huu ulijikita kimahususi katika muundo wa vishazi tegemezi vya Kibukusu. Hivyo, kazi ya Aboh na Essegbey ilirutubisha utafiti huu sana. Ilitoa mwanga katika kubainisha nafasi ya kitenzi katika Kibukusu na jinsi ilivyosaidia kufafanua aina mbalimbali za vishazi tegemezi.

Tafiti za lugha za Kibantu za Afrika Mashariki zinatoa ulinganifu wa karibu zaidi na Kibukusu. Asiimwe (2019) alichunguza kwa undani sifa za kimofosintaksia za vishazi rejeshi katika Runyankore-Rukiga. Alilenga kubainisha aina kuu mbili: vishazi rejeshi vya nomino na vishazi rejeshi vya kishazi. Matokeo yake yalionesha kwamba vishazi rejeshi vya kiima hutambulika kupitia mabadiliko ya toni kwenye kiambishi awali. Vishazi rejeshi vya kiarifu huchukua kiunganishi sharti kilichopatanishwa kinachotenda kama kiunganishi cha Kirai Kishazi. Aidha, alithibitisha kwamba kiambishi cha kuongeza si kiashiria cha vishazi rejeshi kama ilivyodhaniwa awali. Huonesha ukomo wa kishazi kilichowekewa mpaka. Utafiti wa Asiimwe ulitofautiana na utafiti huu. Ulichunguza Runyankore-Rukiga ambayo, ingawa ni lugha ya Kibantu, ina mfumo tofauti wa upatanisho na viunganishi. Utafiti huu ulibainisha vipengele hivi mahususi katika muundo wa Kibukusu. Hata hivyo, utafiti wa Asiimwe ulisaidia utafiti huu. Ulionesha nafasi muhimu ya viunganishi, alama za upatanisho, na alama za ukomo katika uundaji wa vishazi tegemezi.

Kaji (2024) alitafiti uhusiano wa kimuundo kati ya vishazi rejeshi vya kiarifu na vishazi tegemezi vya wakati katika Kinyoro. Madhumuni yake yalikuwa kubainisha jinsi vishazi hivyo vilivyofungamana kimuundo. Alitumia uchambuzi wa toni na vitenzi. Matokeo yalibainisha kwamba vishazi tegemezi vya wakati ni sehemu ya mpangilio mpana wa vishazi rejeshi vya kiarifu. Muundo huu uliweza kujitokeza katika lugha nyingine kama Kijapani. Utafiti wa Kaji ulitofautiana na utafiti huu kiasi. Ulijikita katika uhusiano kati ya aina mbili tu za vishazi katika Kinyoro. Utafiti huu ulichunguza aina mbalimbali za vishazi tegemezi vya vielezi katika Kibukusu kwa upana zaidi. Mwisho, utafiti wa Kaji ulirutubisha utafiti huu. Ulitoa mwanga juu ya uhusiano wa vishazi tegemezi na vishazi rejeshi. Hali hii ilisaidia kuelewa zaidi aina na dhima ya vishazi tegemezi katika Kibukusu.

Mbuki (2019) alitafiti dhana ya ufungamanishaji wa vishazi katika Kisukuma kwa kutumia Nadharia ya Majukumu na Marejeleo. Tija yake ilikuwa kubainisha jinsi vishazi vilivyounganishwa kwa alama za wakati na mwendelezo. Alieleza hali hii kwa kuzingatia kiwango cha kisintaksia. Matokeo yalibainisha kwamba mnyororo wa vishazi ni jambo la kisintaksia linalotokana na ushirikiano wa vishazi vingi. Uunganisho wa pamoja peke yake ndiyo uliosababisha muundo huu katika Kisukuma. Utafiti wa Mbuki ulitofautiana na utafiti huu. Ulichunguza Kisukuma ambayo ni lugha ya Kibantu ya Tanzania. Vilevile, ulitumia Nadharia ya RRG badala ya X-Baa. Kwa hivyo, utafiti wa Mbuki ulisaidia utafiti huu. Ulionesha jinsi vishazi tegemezi vilivyoweza kufungamanishwa vikibeba dhima ya wakati na mwendelezo wa matukio. Dhana hizi zilisaidia

kubainisha nafasi ya kisintaksia ya vishazi tegemezi katika Kibukusu.

Jeremiah (2019) alibainisha aina mbalimbali za vishazi tegemezi katika Kisukuma kwa kutumia Nadharia ya X-Baa. Lengo lake lilikuwa kuonesha jinsi nadharia ya X-Baa inavyosaidia kubainisha miundo ya virai na kueleza mahusiano ya vipashio katika kirai nomino. Matokeo yake yalithibitisha uwezo wa mtazamo huu katika kubainisha nafasi, uhusiano wa vipengele, na taratibu za kimfumo zilizotawala vishazi tegemezi. Utafiti wa Jeremiah ulitofautiana na utafiti huu. Ulichunguza Kisukuma kwa kutumia Nadharia ya X-Baa. Utafiti huu ulichunguza Kibukusu kwa mfumo unaofaa zaidi kwa muundo wa lugha hiyo. Hata hivyo, utafiti wa Jeremiah uliboresha utafiti huu. Ulitoa mfano wa jinsi ya kubainisha muundo wa vishazi tegemezi katika lugha za Kibantu za Afrika Mashariki.

Wakarindi (2018) alitafiti ugumu wa vishazi tegemezi katika Gĩkũyũ kwa kutumia Nadharia ya Sarufi Kazi. Shabaha yake ilikuwa kubainisha uhusiano wa kimaana, kifonolojia, na viashiria vya uhusiano katika muundo wa vishazi changamano. Alitumia data iliyotokana na maandishi na mazungumzo. Matokeo yake yalionesha kwamba vishazi tegemezi vilibeba uhusiano wa upanuzi na uakisi. Hujitokeza kupitia ulinganifu au utegemezi. Vishazi tegemezi vinaweza pia kutekeleza dhima tatu za lugha kwa wakati mmoja kwa sababu ya asili ya mnyambuliko wa Gĩkũyũ. Utafiti wa Wakarindi ulitofautiana na utafiti huu kwa njia fulani. Ulichunguza Gĩkũyũ kwa kutumia Nadharia ya Sarufi Ifaayo. Utafiti huu ulishughulikia Kibukusu kwa mfumo tofauti wa kinadharia. Ingawa lugha zote mbili ni za Kibantu za Kenya. Kwa hivyo, utafiti wa Wakarindi uliufaa utafiti huu. Ulitoa msingi wa kulinganisha matokeo ya Kibukusu na yale ya Gĩkũyũ katika ngazi ya lugha za Kibantu za Afrika Mashariki.

Kwa jumla, Mbuki (2019), Jeremiah (2019), na Wakarindi (2018) wanaafikiana kwamba lugha za Kibantu huwa na aina tatu kuu za vishazi tegemezi: virejeshi, vya kujaza, na vya kielezi. Mwelekeo huu wa aina tatu ndio uliotarajiwa pia kujitokeza katika Kibukusu. Hata hivyo, kama makala hii itakavyoonesha, data za Kibukusu zinaonesha picha changamano zaidi, ikiwa ni pamoja na mgawanyiko wa vishazi vielezi katika aina nne badala ya moja, na uwepo wa aina ya kipekee ya kishazi cha utangulizi ambayo haijabainika waziwazi katika tafiti za awali za Kibukusu, ikiwemo kazi za msingi za Mutonyi (2000), Kisembe (2018), na Watulo (2020), zilizolenga zaidi fonolojia na mofolojia kuliko sintaksia ya kina ya vishazi tegemezi.

Mapitio haya yanaonesha mapengo matatu makuu ya kitaaluma. Kwanza, linahusu eneo la kijiografia na kilugha. Tafiti nyingi za vishazi tegemezi zimejikita katika lugha za Kizungu (Candrasius, 2024; Vogel, 2022; Božić, 2022). Nyingine zimeshughulikia lugha za Kiafrika Magharibi zisizo za Kibantu (Aboh na Essegbey, 2010; Agbo, 2023; Beermann, 2024). Lugha ndogo za Kibantu za Afrika Mashariki, kama Kibukusu, hazijashughulikiwa kikamilifu katika mjadala huu wa kinadharia.

Aidha, pengo la pili linahusu uteuzi wa lugha za Kibantu zenyewe. Tafiti zilizopo za Kibantu (Asiimwe, 2019; Mbuki, 2019; Wakarindi, 2018; Kaji, 2024) zimeegemea lugha kama Runyankore-Rukiga, Kisukuma, Gĩkũyũ, na Kinyoro. Kibukusu kimeachwa nje, licha ya kuwa na wazungumzaji wengi kuliko baadhi ya lugha hizo.

Mwisho ni pengo la kinadharia. Tafiti za awali za Kibukusu (Mutonyi, 2000; Kisembe, 2018; Watulo, 2020) zimeshughulikia fonolojia, mofolojia, na uhamishaji wa vitenzi na maswali ya *wh*-Hazijachambua kwa kina aina za vishazi tegemezi kama kipengele huru cha kisintaksia. Zaidi ya hayo, tafiti hizi, ikiwemo za Kibukusu, zimeainisha vishazi tegemezi kwa vigezo vya kiutendaji-kimaana pekee. Vigezo hivyo hugawa vishazi kulingana na dhima yake ya kisemantiki tu, kama virejeshi, vijaza, au vielezi. Havichunguzi muundo wa ndani wa kisintaksia unaozalisha vishazi hivyo.

Mkabala huu wa kiutendaji-kimaana una udhaifu wa kimsingi. Hauwezi kubainisha kichwa kinachotawala ndani ya kila kishazi. Hauoneshi ni vipengele gani vinavyofungamana moja kwa moja na kichwa hicho kama vijalizo. Hautofautishi hivyo na vipengele vya hiari kama vifafanuzi. Vilevile, hauelezi kama mpangilio wa kihierarkia unabaki sawa katika aina zote za vishazi. Udhaifu huu unadhihirika zaidi katika muundo wa kipekee kama kishazi cha utangulizi, ambacho hakina nafasi katika taipolojia ya awali ya aina tatu (virejeshi, vijaza, vielezi).

Ni pengo hili la kimuundo-kinadharia, zaidi ya ukosefu wa data pekee, ambalo utafiti huu unalenga kuliziba. Nadharia ya X-Baa (Chomsky, 2020; Radford, 1997) inafaa kushughulikia pengo hili. Tofauti na uainishaji wa

kiutendaji-kimaana, nadharia hii inatoa mfumo wa kisarufi-zalishi. Mfumo huu unabainisha kwa usahihi kichwa, kijalizo, na kifafanuzi cha kila kishazi. Unaonesha pia jinsi vipengele hivi vinavyopangwa kihierarkia katika ngazi za X, X′, na X″ (Haegeman, 2020).

Ni uwezo huu wa kuchambua muundo wa ndani, si dhima ya nje pekee, unaoipa nadharia hii nguvu ya kipekee. Inaweza kutoa maelezo ya kimuundo kwa aina za vishazi ambazo hazijawahi kuainishwa hapo awali, kama kishazi cha utangulizi cha Kibukusu. Inaruhusu pia ulinganisho wa kimuundo, si wa kimaana tu, kati ya Kibukusu na lugha nyingine za Kibantu na zisizo za Kibantu zilizotajwa hapo juu (Downing na Marten, 2019).

Hivyo, utafiti huu uliziba mapengo yote matatu. Unatoa uainishaji wa kina wa kwanza wa aina za vishazi tegemezi vya Kibukusu. Uainishaji huu uliegemea nadharia thabiti ya kimuundo. Ulitokana pia na data halisi ya mazungumzo ya wazawa, badala ya kutegemea vigezo vya kiutendaji-kimaana vilivyowekwa mapema kutoka lugha nyingine.

Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya X-Baa, iliyoasisiwa na Noam Chomsky na kusanifiwa na Ray Jackendoff katika miaka ya 1970 (Chomsky, 2020; Radford, 1997). Nadharia hii inadai kwamba kila kirai kina neno kuu (kichwa) kinachosimamia muundo wake wote, huku vipengele vikipangwa katika viwango vya kihierarkia vinavyowakilishwa kwa alama za X, X′, na X″ (Haegeman, 2020). Ndani ya muundo huu, kifafanuzi ni kipengele kinachoongeza maelezo ya ziada kuhusu kichwa bila kuwa cha lazima kimuundo (Cowper, 1992). Kijalizo ni kipashio kinachoungana kwa karibu na kichwa kukamilisha maana yake (Chomsky, 2020). Kipanuzi ni sehemu inayotoa maelezo ya jumla zaidi kuhusu kirai kizima.

Downing na Marten (2019) wanasisitiza kwamba nadharia hii inafaa sana kwa lugha za Kibantu kwa sababu inaweza kufafanua kwa usahihi muundo wa vipashio vya kitenzi, kielezi, na nomino katika sentensi changamano. Katika utafiti huu, kanuni ya kichwa cha kirai ilitumika kwa lengo mahususi. Lengo hilo lilikuwa kubainisha kipashio kinachosimamia kila aina ya kishazi tegemezi cha Kibukusu. Kipashio hiki kinaweza kuwa kiambishi cha urejeshi. Kinaweza pia kuwa kiunganishi cha mahali, cha wakati, au cha sababu. Vilevile, kinaweza kuwa kiunganishi cha masharti. Au kinaweza kuwa kiambishi cha kipekee cha utangulizi. Nadharia hii ina mihimili minne. Mihimili hiyo ni kanuni ya kichwa, upangaji wa kihierarkia, kifafanuzi, na kijalizo. Mihimili hii iliwezesha utambuzi wa vipengele vya msingi vya kila aina ya kishazi. Utambuzi huu ulifanyika kabla ya uchanganuzi wa kina zaidi. Uchanganuzi huo wa kina utafanywa katika sehemu zinazofuata za utafiti. Sehemu hizo zitahusu miundo na sheria za kisarufi.

Kigezo cha kimsingi katika utafiti huu kilikuwa utegemezi wa kisintaksia. Kigezo hiki kinaangalia uwezo wa kishazi kusimama peke yake kama sentensi kamili (Massamba, 2004). Vishazi vyote sita vilivyobainika vilikidhi kigezo hiki. Kila kimoja kilihitaji kishazi kikuu. Bila kishazi kikuu, maana yake haikamiliki kisemantiki wala kisarufi. Kigezo cha pili kilihusu aina ya kiashiria. Kiashiria hiki kinatambulisha kishazi husika. Kinaweza kuwa kiambishi cha urejeshi. Kiambishi hiki hupatana na ngeli, kama ilivyo katika vishazi virejeshi vya lugha nyingi za Kibantu. Kinaweza pia kuwa kiunganishi cha kimuundo. Au kinaweza kuwa kiambishi maalum cha kimofolojia. Kiambishi cha aina hii hubeba maana ya kisemantiki isiyo ya kawaida. Mfano wake ni kishazi cha utangulizi. Vigezo hivi viwili viliongoza uchanganuzi wa data. Kigezo cha kwanza ni utegemezi wa kisintaksia. Kigezo cha pili ni aina ya kiashiria. Kwa pamoja, viliwezesha kubainisha aina sita za vishazi tegemezi vya Kibukusu.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulifuata muundo wa kimaelezo ndani ya mkabala wa kitaamuli, ukilenga kuwasilisha data za kiisimu kwa maneno badala ya vipimo vya kinumerali (Vanderstoep & Johnson, 2008).

Eneo la utafiti lilikuwa Gatuzi Dogo la Sirisia, Kaunti ya Bungoma. Eneo hili liliteuliwa kimakusudi kwa sababu lina wazawa wengi wa jamii ya Wabukusu wenye ufasaha wa hali ya juu wa Kibukusu na wasioathiriwa sana na lahaja nyingine za Kiluhya, hali iliyohakikisha data ziliwakilisha lugha hiyo katika hali yake halisi. Kundi lengwa lilijumuisha wanafunzi wa shule za upili, walimu wa Kiswahili, na wazee wa vijiji hivyo wanaozungumza Kibukusu, wote wakichaguliwa kwa kuzingatia vigezo vya uzawa, ufasaha wa lugha, na uhusiano wao wa moja kwa moja na mada ya utafiti.

Sampuli ya watafitiwa kumi na watano (M1–M15) iliteuliwa kwa njia ya usampulishaji makusudi na mpokezano (Mugenda & Mugenda, 2003). Sampuli iliundwa na makundi matatu, yaliyoteuliwa kwa makusudi. Makundi hayo ni wanafunzi wa shule za upili, walimu wa Kiswahili, na wazee wa jamii ya Wabukusu. Wazee walikuwa na umri wa miaka 57 hadi 75. Jumla ya washiriki walikuwa 15: wanafunzi 7, walimu 5, na wazee 3. Kila kundi liliteuliwa kwa sababu mahususi. Wazee walichaguliwa kwa kuwa wazungumzaji wa asili wenye umri mkubwa zaidi. Wana uzoefu mrefu wa lugha. Usemi wao unaakisi Kibukusu kilichoathiriwa kidogo na mwingiliano wa kisasa wa Kiswahili na Kingereza. Hivyo, walitoa data za kuaminika zaidi kuhusu miundo asili ya vishazi tegemezi. Walimu wa Kiswahili walichaguliwa kwa umahiri wao wa kiisimu. Umahiri huu uliwawezesha kutambua na kubainisha kwa usahihi mipaka ya vishazi tegemezi katika mifano waliyotoa. Wanafunzi walichaguliwa kuwakilisha kizazi kipya cha wazungumzaji. Walisaidia kuonesha kama miundo hiyo bado inatumika sawa katika matumizi ya sasa ya lugha. Mchanganyiko huu uliimarisha uthabiti wa matokeo kupitia mbinu ya pembe tatu. Washiriki wa awali walimsaidia mtafiti kuwatambua watafitiwa wengine waliokidhi vigezo vya ufasaha uliohitajika, mbinu inayofaa hasa pale vyanzo vya data havifahamiki moja kwa moja.

Utafiti ulitumia njia tatu kuu kukusanya data. Njia ya kwanza ilikuwa utafiti wa maktabani. Huu ulihusisha mapitio ya vitabu, majarida, na machapisho ya kitaaluma. Vyanzo hivi vilishughulikia vishazi tegemezi katika lugha za Kibantu, hasa Kibukusu.Njia ya pili ilikuwa ukusanyaji wa data za nyanjani. Data hizi zilipatikana kutoka kwa washiriki 15 kupitia uchunzaji mahuluti na midahalo ya vikundi. Ukusanyaji ulifanyika katika mazingira halisi ya kila siku ya watafitiwa. Maeneo yaliyohusika ni shule za upili za Butonge Boys, Bukokholo Girls, St. Anthony Sirisia, Namang'ofulo, na Bishop Wabukala. Vijiji vinavyozunguka shule hizi, ndani ya Gatuzi Dogo la Sirisia, Kaunti ya Bungoma, pia vilihusika. Mchakato wa ukusanyaji data ulidumu kwa muda wa miezi tatu Kila kikao kilichukua saa nne kwa siku, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kila juma. Vikao vilianza saa tatu asubuhi. Mtafiti alihudhuria mwenyewe ili kuhakikisha uhalisia wa data (Kothari, 2004). Jumla ya tungo 129 zilikusanywa kutoka kwa wazungumzaji wa asili. Tungo hizi ziliwezesha uainishaji wa vishazi kulingana na muundo na kazi zake. Njia ya tatu ilihusisha mchango wa mtafiti binafsi. Mtafiti, akiwa mzungumzaji mzawa wa Kibukusu, alizalisha tungo za ziada kukamilisha data. Umilisi wake wa lugha ulimwezesha kutambua tungo sahihi na zenye makosa (Chomsky, 1986). Data zote zilirekodiwa kwa kanda za sauti na kijidaftari. Baadaye zilitafsiriwa kwa Kiswahili kuwezesha uchambuzi wa kina.

Chombo kikuu cha ukusanyaji data kilikuwa mwongozo wa maswali ya nyanjani wenye maswali kumi na tano (SW1–SW15) yaliyogawanyika kulingana na malengo matatu mahususi ya utafiti mpana zaidi, huku maswali matano ya kwanza (SW1–SW5) yakilenga moja kwa moja kubainisha aina za vishazi tegemezi. Maswali haya yaliwahitaji washiriki kutoa mifano ya sentensi za Kibukusu zenye vishazi tegemezi kutokana na uzoefu wao wa kila siku wa lugha, badala ya kuwapatia orodha ya kategoria za kuchagua, mkabala uliolenga kuepusha upendeleo wa kinadharia na kuruhusu aina halisi za matumizi kujitokeza zenyewe.

Uchanganuzi wa data ulizingatia Nadharia ya X-Baa. Kila mfano ulichunguzwa kwa makini. Lengo lilikuwa kubaini kishazi tegemezi husika. Pia kiambishi au kiunganishi chake kilitambuliwa. Uhusiano wake wa kisintaksia na kishazi kikuu nao ulifafanuliwa (Clarke & Braun, 2014). Kabla ya hapo, data zilipangwa kwa makundi matatu. Hatua hii ilizuia mchanganyiko wa viwango tofauti vya uhalisi wa lugha. Kundi la kwanza lilikuwa mazungumzo ya kawaida. Data hizi zilipatikana kwa uchunzaji mahuluti. Mtafiti alikaa katika mazingira halisi ya watafitiwa. Matumizi yaliyokusanywa yalikuwa ya papo kwa papo, bila mwongozo. Kundi la pili lilitokana na mahojiano na midahalo ya vikundi lengwa. Watafitiwa walijibu maswali yaliyotayarishwa awali. Mbinu hii ililenga moja kwa moja miundo ya vishazi tegemezi iliyokusudiwa. Kundi la tatu lilizalishwa na mtafiti mwenyewe. Kama mzawa wa Kibukusu, aliongeza tungo zilizokosekana. Umilisi wake pia ulitumika kuthibitisha usahihi wa kisarufi wa tungo (Chomsky, 1986). Data za mazungumzo ya kawaida na zile zilizochochewa ziliunda tungo 129. Hizi ndizo zilizounda msingi mkuu wa uchanganuzi. Tungo za mtafiti zilitumika tu kama nyongeza ya kuthibitisha na kuziba mapengo.

Mchakato wa uchanganuzi ulipitia hatua tatu. Hatua ya kwanza ilihusisha kupanga tungo zote kulingana na kiunganishi au kiambishi kilichojitokeza. Pili, mchakato huu ulihusisha kulinganisha tungo zenye kiashiria kimoja. Lengo lilikuwa kubaini kama zinaunda aina moja

au zaidi ya kishazi tegemezi. Tungo za ziada za mtafiti ziliziba pengo pale ambapo data za nyanjani hazikutosha. Hatua ya mwisho ilirejesha aina zilizopatikana kwenye maswali ya utafiti. Pia zilirejeshwa kwenye misingi ya Nadharia ya X-Baa. Hatua hii iliimarisha uthabiti wa kinadharia. Umilisi wa mtafiti kama mzawa (Chomsky, 1986) ulihakiki usahihi wa kisarufi wa kila kategoria. Msisitizo ulikuwa kubaini aina za vishazi na jinsi vinavyojitokeza kimatumizi. Data halisi za wazawa, hasa za mazungumzo na zilizochochewa, ndizo zilizotawala. Kategoria za kinadharia zilizowekwa awali hazikutegemewa kikamilifu. Mkabala huu uliwezesha kuibuka kwa aina ya kishazi cha utangulizi. Aina hii haikutarajiwa kabla ya ukusanyaji wa data.

MATOKEO YA UTAFITI

Data kutoka kwa washiriki kumi na watano zilibainisha aina sita kuu za vishazi tegemezi. Jedwali la 1 linatoa muhtasari wa aina hizi, kabla ya ufafanuzi wa kina wa kila moja. Uainishaji huu ulitegemea vigezo vitatu vinavyokamilishana. Hakukuwa na kigezo kimoja pekee. Kigezo cha kwanza kilikuwa cha kimofolojia. Kila aina ya kishazi ilitambuliwa na kundi lake mahususi la viambishi au viunganishi. Vikundi hivi havikuingiliana. Kishazi kirejeshi kinaongozwa na viambishi vya urejeshi *oyo/abo, syo/sio/byo/bio*. Kishazi cha wakati kinaongozwa na viunganishi na maneno ya wakati *bise, likoloba, chisaa*. Kishazi cha sababu kinaongozwa na viunganishi vya kisawa *khubela/sikila*. Kishazi cha masharti kinaongozwa na *niba/kaba* au *mbanga*. Kishazi cha mahali kinaongozwa na kiunganishi *abundu nio*. Kishazi cha utangulizi kinaongozwa na kiambishi cha kipekee *nekhanja/nekharakikha*.Aidha, kigezo cha kisintaksia, kikiegemea Nadharia ya X-Baa. Kila kiambishi au kiunganishi kilichambuliwa kama kichwa cha kisintaksia kinachosimamia muundo wa kishazi husika. Aina za vishazi zilitofautishwa kulingana na kichwa hiki cha kimuundo. Uwepo wa neno fulani pekee haukutosha kutofautisha aina.

Mwisho, Kigezo cha kimaana kilitumika. Kila aina ilibeba uhusiano tofauti wa kisemantiki kati ya kishazi tegemezi na kishazi kikuu. Uhusiano huu ulijumuisha urejeleo, mahali, wakati, sababu, sharti, au mpangilio wa kimantiki wa matukio. Vigezo hivi vitatu vilithibitishwa kupitia mbinu ya pembe tatu. Washiriki wote kumi na watano walitoa mifano inayoakisi aina hizi sita, bila kuelekezwa na mtafiti. Matokeo yaliendana na mfumo wa Nadharia ya X-Baa. Yaliendana pia na tafiti linganishi za lugha nyingine za Kibantu (Jeremiah, 2019; Asiimwe, 2019; Wakarindi, 2018; Kaji, 2024).

Jedwali 1. Muhtasari wa Aina za Vishazi Tegemezi vya Kibukusu

Aina ya Kishazi	Kiashiria/Kiambishi	Mfano (KBKS)	Tafsiri
Kirejeshi	*oyo*/*abo*, *syo*/*byo*	*Omwana oyo walilile alola esikuli*	Mtoto aliyelia atafika shuleni
Cha mahali	*abundu nio* / *abundu ne-*	*Nachile abundu neabele*	Nilikwenda mahali alikuwa
Cha wakati	*bise*/*nenaba*; *likoloba*, *chisaa*	*Bise nibyo bachilile akonile*	Wakati walipokwenda, alilala
Cha sababu	*khubela* / *sikila*	*Khubela achelewe alomane*	Kwa sababu alichelewa, alihasimu
Cha masharti	*kaba*/*niba; mbanga*	*Kaba olola olabona omwana*	Kama utafika utaona mtoto
Cha utangulizi	*nekhanja* / *nekharakikha*	*Nekhanja khulima, nalola kumukunda khuranga*	Kabla ya kulima, nilitazama shamba kwanza

Kishazi Kirejeshi

Washiriki wote 15 walitaja kishazi kirejeshi mara nyingi zaidi. Kishazi hiki kinatambulika kwa kiambishi cha urejeshi. Kiambishi hicho hubadilika kulingana na ngeli na idadi ya nomino. Kwa mtu mmoja hutumika *oyo*. Kwa watu wengi hutumika *abo*. Kwa kitu kimoja hutumika *syo*. Kwa vitu vingi hutumika *byo*. Mifano ni pamoja na "*Omukhasi oyo watekhile byakhulia awele*" (Mwanamke aliyepika chakula amekwisha). Mfano mwingine ni

"*Omusomi oyo asomile abira*" (Mwanafunzi aliyesomea alifaulu).

Matokeo haya yanaafikiana na fasihi ya awali kwa njia mbili. Kwanza, utawala wa kirejeshi unathibitisha madai ya Mutonyi (2000) na Kaji (2024). Wao walidai kirejeshi ni aina tawala ya vishazi tegemezi katika Kibantu. Pili, upatanisho wa kiambishi na ngeli unafanana na matokeo ya Asiimwe (2019) katika Runyankore-Rukiga. Naye alibaini upatanisho kama huo. Hii ni ushahidi kwamba upatanisho wa ngeli ni sifa thabiti ya Kibantu kwa jumla. Hata hivyo, kuna eneo moja la utata. Katika Runyankore-Rukiga, toni pekee zinaweza kutambulisha kirejeshi. Kiambishi cha wazi hakihitajiki wakati huo. Kibukusu ni tofauti. Data zake zinaonesha utegemezi mkubwa wa viambishi vya wazi: *oyo, abo, syo,* na *byo*. Hata hivyo, washiriki wanne M5, M9, M12, na M14 walisema toni nazo zina mchango. Kauli hii inaleta utata fulani. Haiwezekani kuhitimisha kwa uhakika kwamba viambishi vya wazi ndiyo njia pekee ya utambulisho.

Tofauti hii inaweza kuelezwa kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni kisintaksia. Upatanisho wa kiambishi na nomino si suala la kimofolojia tu. Ni sheria inayounganisha sehemu mbili za sentensi. Kiambishi hufanya kazi ya kichwa cha muundo, kwa mujibu wa Nadharia ya X-Baa. Kichwa hiki hakiwezi kuachwa. Ndiyo maana kirejeshi kinajibu swali la "ni nani?". Kinafafanua nomino. Hii ni tofauti na vielezi, vinavyojibu maswali ya vipi, lini, au wapi. Sababu ya pili inahusu mfumo wa lugha. Kibukusu tayari kina mfumo dhabiti wa viambishi vya wazi. Kwa sababu hiyo, toni inaonekana kuwa nyongeza ya kusisitiza. Si njia kuu ya utambulisho. Hali hii ni tofauti na Runyankore-Rukiga. Kwa mujibu wa Asiimwe, huko toni pekee zinaweza kubeba mzigo mzima. Hii hutokea pale kiambishi cha wazi kikikosekana.

Unyumbufu wa kimuundo unaonekana pia katika mfano mwingine. Mfano huo ni "*Omwana oyo watekha akhola bulayi*" (Mtoto ambaye alipika alifanya vizuri). Mfano huu unaonesha kishazi kirejeshi kinaweza kudadavuliwa zaidi na kielezi. Hii hutokea bila kupoteza dhima yake ya msingi. Kishazi kinabaki chini ya udhibiti wa kiambishi kimoja cha urejeshi.

Kwa jumla, kirejeshi cha Kibukusu kina sifa nne za msingi. Kwanza, kiambishi chake ni kichwa kisichoweza kuachwa. Pili, kina upatanisho wa ngeli na idadi kama sheria ya kisintaksia. Tatu, kina utegemezi wa kisintaksia usio na budi kwa kishazi kikuu. Nne, kina dhima ya kufafanua nomino. Sifa hizi zinaonesha jambo muhimu. Kirejeshi si tu aina inayotumika mara nyingi. Ni pia kielelezo bora cha ufanisi wa Nadharia ya X-Baa. Mwishowe, mchango wa toni uliotajwa na baadhi ya washiriki unafungua eneo jipya la utafiti. Tafiti zijazo zinaweza kuchunguza kwa kina jinsi toni na viambishi vya wazi vinavyoshirikiana. Hii itasaidia kuelewa vyema utambulisho wa vishazi virejeshi vya Kibukusu.

Kishazi cha Mahali

Kishazi cha mahali cha Kibukusu kina utofauti wa kisemantiki wa ndani. Utofauti huu haupo katika Kiswahili Sanifu. Kiunganishi *abundu nio* kinaonesha mahali pa tendo la sasa au la baadaye. Kiunganishi *abundu ne-* au *abundu neabele* kinaonesha mahali pa tendo lililopita. Mfano ni "*Nachile abundu neabele*" (Nilikwenda mahali alikuwa). Kishazi hiki kina nafasi yake ya kawaida. Nafasi hiyo ni baada ya kishazi kikuu. Hata hivyo, kinaweza kuhamishwa mbele kwa madhumuni ya msisitizo. Kishazi hiki kinahusiana na kitenzi cha kishazi kikuu. Hakihusiani na nomino.

Matokeo haya yanaafikiana na tafiti mbili za awali. Kwanza, yanathibitisha madai ya Van de Velde (2019). Yeye alieleza kuwa Kibukusu kina kanuni maalum za kupanga vipashio vya mahali. Kanuni hizo hazipo katika lugha nyingi za jirani. Pili, yanaunga mkono hoja ya Mbuki (2019). Yeye alisema vipengele vya mahali vinahusiana na mfumo wa wakati katika Kisukuma.

Kwa hivyo, kuna tofauti muhimu ndani ya ufanani huu. Kiswahili Sanifu na lugha nyingi za jirani hutumia kiunganishi kimoja tu cha jumla, kama "ambapo". Mbuki naye alieleza uhusiano wa jumla wa mahali na wakati, bila utaratibu maalum wa kisarufi. Kibukusu ni tofauti. Uchaguzi kati ya *abundu nio* na *abundu ne-* pekee ndio hubeba habari ya wakati. Hakuna haja ya kiambishi cha ziada.

Tofauti hii inaelezeka kisayansi. Kiunganishi cha mahali cha Kibukusu si alama ya mahali pekee. Ni pia kichwa cha kisintaksia. Kichwa hicho hubeba sifa ya wakati, kwa mujibu wa Nadharia ya X-Baa (Radford, 1997). Hali hii haipo katika Kiswahili Sanifu. Huko, mahali na wakati huonyeshwa kwa vipashio viwili tofauti.

Uhamishaji wa kishazi hiki nao una maelezo. Kwa mfano, "*Omwana akonile abundu aoo*" inaweza kubadilika kuwa *"Abundu aoo amwana akonileo*".

Mabadiliko haya si ya kiholela. Yanadhibitiwa na malengo ya kimawasiliano. Hutokea pale mahali ndipo habari mpya inayostahili msisitizo. Hoja hii inaendana na mtazamo wa Massamba (2004). Yeye alisema muundo wa kishazi tegemezi unaongozwa na malengo ya mawasiliano, si sheria za mpangilio pekee.

Uvumbuzi huu una maana mbili. Kwanza, Kibukusu kinabeba habari za wakati ndani ya kishazi cha mahali. Uwezo huu haujitokezi wazi hata katika lugha za jirani zilizosomwa zaidi. Huu ni ushahidi zaidi wa utajiri wa kimuundo uliotajwa na Van de Velde. Pili, uhusiano wa mahali na wakati unaweza kuchukua sura tofauti kutoka lugha moja hadi nyingine. Hii inathibitisha umuhimu wa kuendelea kuchunguza lugha ndogo za Kibantu kwa kina, badala ya kuridhika na jumla za kikanda.

Kishazi cha Wakati

Kishazi cha wakati cha Kibukusu kinaanzishwa kwa njia mbili. Njia ya kwanza ni viunganishi vya kimuundo. Mfano ni *bise* au *nenaba*. Viunganishi hivi huanzisha kishazi kamili. Kishazi hicho kina kiima na kiarifu vyake. Mfano ni "*Bise nibyo bachilile akonile"* (Wakati walipokwenda, alilala). Njia ya pili ni vielezi vya wakati. Mfano ni *likoloba* (jana) au *chisaa chitaru* (saa tatu). Vielezi hivi ni vya hiari. Vinaongeza tu habari ya wakati. Havijiunda kishazi chenye kiima chake. Mfano ni "*Olile chisaa chitaru*" (Alifika saa tatu). Kishazi hiki kina nafasi yake ya kawaida. Nafasi hiyo ni baada ya kishazi kikuu. Hata hivyo, kinaweza kutangulia kishazi kikuu. Hii hutokea pale wakati ndipo habari mpya inayostahili msisitizo. Sifa hii inafanana na ile ya kishazi cha mahali.

Matokeo haya yanahusiana na tafiti mbili za awali. Kwanza, mgawanyo wa aina mbili unaendana na Mwamzandi (2022). Yeye alibainisha aina hizo hizo katika mabadiliko ya kishazi cha wakati cha Kiswahili. Pili, Candrasius (2024) alisema vishazi vya wakati ndivyo aina tawala katika lugha nyingi alizozichunguza. Hata hivyo, hoja ya pili inahitaji ufafanuzi. Data ya Kibukusu haiungi mkono kikamilifu madai ya Candrasius. Katika utafiti huu, kishazi kirejeshi ndicho kilichotajwa mara nyingi zaidi. Kishazi cha wakati hakikuwa cha kwanza. Hata hivyo, ndani ya kundi la vielezi pekee; mahali, wakati, sababu, na masharti; kishazi cha wakati kilitokea kwa wingi zaidi. Kwa hiyo, matokeo yanaafikiana na Candrasius, lakini kwa kiwango finyu zaidi kuliko madai yake ya jumla.

Tofauti hii ina maelezo mawili. Kwanza, tofauti kati ya kiunganishi cha kimuundo na kielezi cha hiari si ya kileksika tu. Ni tofauti ya kimsingi kisarufi, kwa mujibu wa Mwamzandi (2022). Kiunganishi cha kimuundo huunda kishazi chenye hadhi kamili. Kina kiima chake. Kielezi cha hiari hakina hadhi hiyo. Kinabaki kipashio cha ziada. Tofauti hii inaendana na kanuni za Nadharia ya X-Baa. Nadharia hii inatofautisha kirai kamili na kifafanuzi cha hiari (Radford, 1997). Vilevile, kutokuafikiana na Candrasius kwa ujumla kuna sababu ya kiutendaji. Katika data ya Kibukusu, kufafanua nomino ni hitaji la mawasiliano linalojitokeza mara kwa mara. Hitaji hili linazidi lile la kubainisha wakati mahususi. Hii ni tofauti ya kimatumizi, si mgongano wa kimuundo.

Ugunduzi huu una maana mbili. Kwanza, madai ya jumla kutoka lugha nyingine hayawezi kuchukuliwa moja kwa moja. Madai kama ya Candrasius kuhusu utawala wa vishazi vya wakati yanahitaji uthibitisho dhidi ya data mahususi za kila lugha. Msisitizo huu unaendana na hoja kuu ya makala hii. Pia, kuna mfano unaoonesha mwingiliano wa aina mbili za vishazi. Mfano ni "*Nebakhamala khulia, bemile"* (Kabla hawajamaliza kula, walisimama). Mfano huu unabeba habari ya wakati. Vilevile, unabeba mpangilio wa kimantiki wa matukio mawili. Hii inaashiria uhusiano wa karibu kati ya kishazi cha wakati na kishazi cha utangulizi. Kishazi cha utangulizi kitajadiliwa baadaye. Dalili hii inaonesha kuwa mipaka kati ya aina hizi mbili si migumu katika Kibukusu.

Kishazi cha Sababu

Kishazi cha sababu cha Kibukusu huanzishwa na viunganishi viwili. Viunganishi hivyo ni *khubela* na *sikila*. Vyote vina maana ya "kwa sababu". Mfano ni "*Khubela achelewe alomane*" (Kwa sababu alichelewa, alihasimu). *Sikila* hutumika zaidi na wazee. Hii ni ushahidi wa tofauti ya kiisimujamii au ya kizazi. Si tofauti ya kisarufi. Mpangilio wa kishazi hiki si wa lazima. Kinaweza kutangulia au kufuata kishazi kikuu. Uchaguzi huu unategemea msisitizo wa habari. Mfano wa kwanza ni "*Khubela alwile, akonile*" (Kwa sababu alichoka, alilala). Mfano wa pili ni "*Alila khubela aumia*" (Alilia kwa sababu aliumia). Katika mifano yote, kiunganishi *khubela* au *sikila* kinabaki cha lazima.

Matokeo haya yanahusiana na tafiti mbili za awali. Kwanza, uwepo wa kishazi cha sababu kama aina huru unaunga mkono Candrasius (2024). Yeye alibainisha

vishazi vya sababu kama moja ya aina kuu tatu za vishazi tegemezi. Pili, uwepo wa polisemia unaunga mkono Božić (2022). Yeye alionesha katika Kiingereza na Kikroeshia kwamba viunganishi vya wakati vinaweza pia kubeba maana ya sababu. Hata hivyo, kuna utata unaostahili kutiliwa maanani. Kiunganishi *bise* kiliainishwa kama kiunganishi cha msingi cha wakati. Lakini katika baadhi ya miktadha, kilibainika kubeba maana ya sababu pia. Jambo hili linaibua swali muhimu. Je, mstari kati ya kishazi cha wakati na kishazi cha sababu ni thabiti? Au unategemea zaidi muktadha wa matumizi?

Utata huu una maelezo mawili yanayohusiana. Kwanza, uwepo wa viunganishi viwili vya kisawa unaonesha jambo moja. Tofauti za kimatamshi zinaweza kutokea bila kuathiri kazi ya kisintaksia ya kiunganishi. Kiunganishi hubaki kichwa cha kishazi, kwa mujibu wa Nadharia ya X-Baa (Radford, 1997). Kwa hiyo, tofauti ya kiisimujamii na tofauti ya kisintaksia ni vitu viwili tofauti. Havitegemeani.

Aidha, polisemia ya *bise* ina maelezo ya kidhana. Matukio yanayofuatana kwa wakati mara nyingi huonekana kubeba uhusiano wa sababu. Tendo la kwanza huonekana kusababisha hali ya pili. Kwa sababu hiyo, kiunganishi kimoja cha wakati kinaweza kubeba dhima ya sababu pia. Hakihitaji kiambishi tofauti. Hali hii inaendana na madai ya Božić. Yeye alisema polisemia ya aina hii ni kipengele cha ulimwengu wa lugha kwa jumla.

Mchango huu una maana mbili. Kwanza, unaongeza ushahidi mpya wa Kiafrika kwa hoja ya Božić. Hoja hiyo kuhusu polisemia haikomei lugha za Kizungu pekee. Aidha, unaonesha jambo muhimu kuhusu uainishaji wa aina sita za Kibukusu. Ingawa una manufaa makubwa ya kimuundo, si mfumo wenye mipaka migumu kati ya kategoria. Jambo hili linahitaji tahadhari katika matumizi ya vitendo, kama ufundishaji. Pia linafungua eneo jipya la utafiti wa kisemantiki katika tafiti zijazo.

Kishazi cha Masharti

Kishazi cha masharti cha Kibukusu kina aina mbili ndogo. Aina hizi zinatofautiana kimuundo. Aina ya kwanza ni sharti linalowezekana. Sharti hili hutumia viunganishi *kaba* au *niba*. Viunganishi hivi huambatana na wakati ujao (-la-). Wakati huu huonekana katika vishazi vyote viwili. Mfano ni "*Kaba olola olabona omwana*" (Kama utafika utaona mtoto). Aina ya pili ni sharti la dhana. Sharti hili halowezekani kimatendo. Hutumia kiambishi *mbanga*. Kiambishi hiki huambatana na mabadiliko ya viambishi vya wakati uliopita. Mfano ni "*Mbanga nakhalibele ne chisendi, nakhalikulile ekhafu*" (Kama ningalikuwa na pesa, ningelinunua ng'ombe). Mpangilio wa kishazi hiki ni wa lazima. Kishazi cha masharti hutangulia kishazi kikuu. Kiunganishi *kaba* au *niba* ni kipashio cha lazima. Hakiwezi kudondoshwa.

Matokeo haya yanaafikiana na tafiti mbili za awali. Kwanza, mgawanyo huu unathibitisha madai ya Palmer (2001). Yeye alisema tofauti ya sharti-linalowezekana na sharti-la-dhana ni kipengele cha kisarufi cha kiulimwengu. Pili, matokeo yanaendana na Nyandago (2013). Yeye alibainisha muundo unaofanana katika Ekegusii na Kiswahili Sanifu. Huko, viambishi -nge- na -ngali- hutekeleza kazi inayolingana na *mbanga* cha Kibukusu. Kwa maneno mengine, tofauti hii hubebwa na mofolojia ya kitenzi. Si kiunganishi.

Vilevile, kuna tofauti muhimu ndani ya ufanani huu. Kiswahili Sanifu kinatumia mkakati ule ule wa kimofolojia. Lakini bado kina viunganishi vingi vya kileksika. Mfano ni kama, ikiwa, iwapo, na endapo. Viunganishi hivi vina tofauti ndogo za kimaana. Kibukusu ni tofauti. Kinatumia jozi moja tu ya viunganishi vya kisawa, *kaba* na *niba*, kwa hali zote mbili. Hii ni tofauti ya wazi kutoka lugha yake dada ya kikanda.

Tofauti hii ina maelezo. Kibukusu kinaonekana kuweka kazi nzima ya kutofautisha masharti kwenye kiambishi cha kitenzi. Haigawanyi kazi hiyo kati ya kiunganishi na kitenzi, tofauti na Kiswahili. Kwa mtazamo wa Nadharia ya X-Baa, kiunganishi *kaba*/*niba* kinabaki kichwa thabiti cha kishazi. Sifa za kimaana; uwezekano dhidi ya udhanifu huhesabiwa ngazi ya chini zaidi. Ngazi hiyo ni kwenye kitenzi chenyewe (Chomsky, 2020; Radford, 1997). Kisembe (2018) naye alithibitisha jambo hili. Alisema mfumo huu ni tofauti ya kisintaksia ya kina. Si ya kileksika tu. Sababu ni kwamba viambishi vya kitenzi hubadilika kwa muundo mzima wa kishazi. Havibadiliki kwa neno moja tu.

Mchango huu una maana mbili. Kwanza, Kibukusu kinashiriki na Ekegusii mfumo wa kisintaksia unaotegemea mofolojia ya kitenzi. Mfumo huu ni kielelezo cha kundi la lugha za Kibantu za Afrika Mashariki. Unatofautiana na mkakati wa Kiswahili Sanifu, ulio na utajiri zaidi wa kileksika. Huenda tofauti

hii inatokana na mwingiliano mkubwa wa kihistoria wa Kiswahili na lugha nyingine. Aidha, kuna faida ya kiutendaji. Mfumo rahisi wa kiunganishi kimoja unamaanisha jambo muhimu. Wanafunzi wa Kibukusu hawahitaji kukariri viunganishi vingi. Wanahitaji tu kumudu mfumo mmoja wa mabadiliko ya kiambishi cha kitenzi. Jambo hili lina manufaa ya moja kwa moja. Manufaa hayo yanahusu ufundishaji na uhifadhi wa lugha.

Kishazi cha Utangulizi

Kibukusu kina kishazi cha kipekee. Kishazi hiki hutumia viambishi shirikishi *nekhanja* na *nekharakikha*. Vyote vina maana ya "kabla ya". Kishazi hiki kina mpangilio wa kimantiki tofauti na kishazi cha kawaida cha wakati. Tendo linalotajwa kwanza ndilo linaloongoza kiakili tendo la kishazi kikuu. Hii hutokea hata kama, kwa wakati halisi, tendo hilo hutokea baadaye. Mfano bora ni "*Nekhanja khulima, nalola kumukunda khuranga*" (Kabla ya kulima, nilitazama shamba kwanza). Washiriki wanne M1, M4, M9, na M13 walitoa mifano inayolingana. Washiriki hawa wana asili, umri, na taaluma tofauti. Hawakuelekezana. Hii ni ushahidi imara kwamba muundo huu ni sehemu halisi ya umilisi wa asili wa Kibukusu.

Matokeo haya yanahusiana na tafiti mbili za awali. Tafiti hizo zinahusu mpangilio wa matukio katika lugha za Kibantu za Afrika Mashariki. Mbuki (2019) alibainisha kwamba, katika Kisukuma, mnyororo wa vishazi unaoonesha mpangilio wa matukio ni jambo la kina kisintaksia. Wakarindi (2018) naye alibainisha, katika Gĩkũyũ, kwamba vishazi vya wakati vinahusiana kwa karibu na mpangilio wa matukio. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa ndani ya ufanani huu. Tofauti hii ndiyo inayofanya data ya Kibukusu kuwa mchango wa kipekee. Wala Mbuki wala Wakarindi hawakubainisha kiambishi maalum kinachosimamia mpangilio huu. Wote waliripoti jambo hili kama tabia ya jumla ya kimuundo. Hawakukiona kama kishazi chenye kiambishi chake mahususi. Kwa maneno mengine, Kibukusu hakiishii kuafikiana na hoja ya tafiti hizo mbili. Kinaipita. Kinatoa ushahidi wa kwanza wazi wa kiambishi kilichojitolea kikamilifu kwa dhima hii.

Tofauti hii ina maelezo. Kisukuma na Gĩkũyũ, kwa mujibu wa maelezo yaliyopo, hazina kichwa maalum cha aina hii. Kibukusu kimeendeleza kichwa maalum cha kisintaksia, yaani *nekhanja*/*nekharakikha*. Kichwa hiki hubeba peke yake dhima nzima ya kuashiria mpangilio wa kimantiki. Haiachii dhima hiyo ibebwe na muktadha. Wala haiachii ibebwe na viunganishi vya kawaida vya wakati, kama *bise* au *nenaba*. Hii inaendana na Nadharia ya X-Baa (Chomsky, 2020; Radford, 1997). Uwepo wa kiambishi hiki unaonesha jambo muhimu. Mpangilio wa kimantiki katika Kibukusu si suala la kimaana pekee. Umeingizwa moja kwa moja katika sarufi. Ni kichwa cha kishazi kisichoweza kuachwa. Hali hii inafanana na jinsi *khubela* au *sikila* kinavyofanya kazi katika kishazi cha sababu.

Uvumbuzi huu una maana kubwa mbili. Kwanza, mchango wa makala hii si kuthibitisha jambo lililokwisha julikana. Mchango wake ni kuongeza kipengele kipya cha kisarufi. Kipengele hiki hakijawahi kubainika katika fasihi ya lugha za Kibantu za Kenya. Vilevile, Kibukusu kinaonesha uwezo mkubwa licha ya kuwa na fasihi ndogo ya kiisimu. Kinaweza kuchangia data zinazokwenda mbali zaidi ya zile za lugha jirani zilizosomwa zaidi, kama Kisukuma na Gĩkũyũ. Huu ni ushahidi imara wa hoja kuu ya makala hii. Lugha ndogo za Kibantu zinahitaji kuchunguzwa kimahususi. Haziwezi kudhaniwa kubeba tu miundo iliyokwisha julikana kutoka lugha kubwa zinazohusiana nazo.

Sifa za Jumla za Vishazi Tegemezi vya Kibukusu

Kwa jumla, aina sita za vishazi tegemezi vya Kibukusu zina sifa nne za pamoja. Kwanza, kila aina ina kiashiria chake cha kisintaksia. Kiashiria hiki kinaitofautisha na aina nyingine. Jambo hili linaendana na kanuni ya kichwa cha kirai katika Nadharia ya X-Baa.Pia, vishazi vyote sita vinakidhi utegemezi wa kisintaksia. Aidha, vishazi vine; mahali, wakati, sababu, na utangulizi vina unyumbufu wa mpangilio. Unyumbufu huu unadhibitiwa na msisitizo wa habari. Kinyume chake, vishazi viwili; kirejeshi na masharti vina mpangilio thabiti zaidi. Mwisho, jozi za viunganishi vinavyofanana *(khubela/sikila; nekhanja/nekharakikha)* hazitofautiani kisarufi. Tofauti yake ni ya kiisimujamii au ya kizazi.

Kuhusu makundi ya msingi, matokeo yanaafikiana na fasihi ya awali ya Kibantu. Mbuki (2019), Jeremiah (2019), na Wakarindi (2018) waliripoti aina tatu za msingi katika Kisukuma na Gĩkũyũ: virejeshi, vijaza, na vielezi. Mutonyi (2000) na Kaji (2024) walidai kishazi kirejeshi ni aina tawala katika Kibantu kwa jumla. Data ya Kibukusu inaunga mkono hoja hiyo moja kwa moja. Washiriki wote 15 walitaja kishazi kirejeshi mara nyingi zaidi. Hii inaeleweka kwa sababu kufafanua nomino ni hitaji la kawaida la mawasiliano. Hitaji hilo linajitokeza

zaidi kuliko uhusiano mahususi kama sababu au masharti. Kwa hiyo, muundo wa msingi wa vishazi tegemezi unaonekana kuwa sifa thabiti ya lugha za Kibantu. Hii inaimarisha uhalali wa kutumia X-Baa katika kuchanganua lugha mbalimbali za kundi hili.

Hata hivyo, muundo wa ndani wa kundi la vielezi haufanani na matarajio hayo. Mbuki (2019), Jeremiah (2019), na Wakarindi (2018) walichukulia vielezi kama kundi moja. Utafiti huu ulionesha tofauti. Vielezi vya Kibukusu vinagawanyika katika aina nne: mahali, wakati, sababu, na masharti. Kila aina ina kiambishi chake na sheria zake za mpangilio. Sababu ya utata huu ni matumizi ya Kibukusu ya viambishi tofauti kwa kila uhusiano wa kisemantiki. Hali hii tofauti na baadhi ya lugha zilizosomwa awali, ambazo hutumia kiunganishi kimoja cha jumla. Kigezo cha kimofolojia kilichotumika katika utafiti huu ndicho kilichowezesha ugunduzi huu. Tafiti za awali zilitegemea zaidi vigezo vya kimaana. Matokeo haya yanaonesha kuwa Kibukusu kina utajiri wa kisintaksia unaozidi mfumo rahisi wa aina tatu. Hali kadhalika, lugha nyingine ndogo za Kibantu zinaweza kuwa na utajiri kama huo. Mifumo ya uainishaji iliyojengwa kutoka lugha chache haipaswi kuchukuliwa kama kiwango kisichobadilika.

Mchango mkubwa zaidi wa utafiti huu ni kishazi cha utangulizi (*nekhanja/nekharakikha*). Kishazi hiki hakikubainika katika tafiti za awali za Kibukusu (Mutonyi, 2000; Kisembe, 2018). Pia hakikubainika katika tafiti nyingine za lugha za Kibantu za Kenya. Mbuki (2019) alieleza mnyororo wa vishazi unaoonesha mpangilio wa matukio katika Kisukuma. Wakarindi (2018) alibainisha uhusiano kama huo katika Gĩkũyũ. Hata hivyo, hakuna aliyebainisha kiambishi maalum kinachosimamia hali hii pekee. Hii si tofauti ndogo. Ni ongezeko jipya kwenye typolojia iliyokuwepo. Kutokubainika kwake awali kunaweza kutokana na hali yake ya kitamaduni.

Kiambishi hiki kinahusiana na maarifa mahususi, kama upangaji wa kazi za kilimo. Kwa sababu hiyo, kinaweza kukosa kubainika na mtafiti asiyekuwa mzawa. Vilevile, kinaweza kukosa kubainika bila mbinu za kina za data za nyanjani. Nafasi ya mtafiti kama mzungumzaji mzawa ilichangia moja kwa moja ugunduzi huu. Ugunduzi huu una mchango mkubwa wa kisayansi kwa fasihi ya isimu ya Kibantu. Pia unathibitisha umuhimu wa data halisi za wazawa kuliko kutegemea makundi ya kinadharia pekee. Kinadharia, matokeo haya yanathibitisha uwezo wa Nadharia ya X-Baa. Downing na Marten (2019) walipendekeza uwezo huu kwa lugha za Kiafrika. Kila aina ya kishazi kilichobainika kina kichwa cha kisintaksia kinachosimamia muundo wake. Hii ni sawa iwe ni kiambishi cha urejeshi, cha mahali, cha wakati, cha sababu, cha masharti, au cha utangulizi. Muundo huu unaendana na kanuni za msingi za X-Baa (Chomsky, 2020; Radford, 1997). Matokeo haya yanaunga mkono hoja ya Aboh na Essegbey (2010) na Agbo (2023). Wao wanasema lugha za Kiafrika zinahitaji uchambuzi unaozingatia sifa zake maalum. Vigezo vilivyojengwa kwa lugha za Kizungu pekee havitoshi. Hii inaonesha kwamba X-Baa, ikitumika kwa unyumbufu, inaweza kufaa hata kwa lugha ndogo za Kibantu.

Kwa kulinganisha na lugha nyingine za Afrika Mashariki, kuna ufanani na tofauti. Kama ilivyo katika Runyankore-Rukiga (Asiimwe, 2019), kishazi kirejeshi cha Kibukusu kinapatana kisarufi na ngeli ya nomino husika. Hii inaonesha kuwa upatanisho wa ngeli ni sifa thabiti ya Kibantu kwa jumla. Hata hivyo, kuna tofauti moja muhimu. Katika Runyankore-Rukiga, toni pekee zinaweza kutambulisha vishazi rejeshi. Kibukusu kinategemea zaidi viambishi vya wazi. Ijapokuwa washiriki M5, M9, M12, na M14 walisema toni pia zina mchango.

Hoja hii inaendana na Mutonyi (2000). Vilevile, kishazi cha wakati cha Kibukusu kinatofautiana na cha Kiswahili Sanifu (Mutonyi, 2000; Watulo, 2020). Kibukusu kinatofautisha wakati wa karibu na wa mbali kwa viambishi maalum. Kiswahili hakina utofautishaji kama huo. Tofauti hizi zinaonesha kuwa lugha za Kibantu zinaweza kutofautiana kwa kina hata ndani ya eneo moja. Hii ni ushahidi wa umuhimu wa tafiti za lugha mahususi kuliko jumla za kikanda.

Ni muhimu pia kutambua mipaka ya matokeo haya. Vogel (2022) alionesha katika Kijarawara kwamba uainishaji wa vishazi tegemezi hutegemea vigezo vya mtafiti. Vigezo tofauti vinaweza kuzalisha idadi tofauti za aina. Kwa hiyo, aina sita zilizobainika hapa si orodha kamili ya vishazi vyote vya Kibukusu. Tofauti ndogo za kilahaja zilijitokeza hata ndani ya sampuli hii. Hasa kuhusu viambishi vya wakati wa mbali uliopita. Hii ni ushahidi kwamba Kibukusu, kama lugha zote hai, kina utofauti wa asili. Hata hivyo, kuna uthibitisho imara kupitia mbinu ya pembe tatu. Washiriki wasioelekezana walitoa mifano inayofanana.

Hasa kishazi cha utangulizi, kilichotolewa na washiriki wanne wa asili tofauti. Hii inathibitisha kwamba aina sita zinawakilisha umilisi halisi wa wazawa. Si uzushi wa kiakademia wa mtafiti. Kiutendaji, matokeo haya yana umuhimu kwa walimu wa Kiswahili. Aidha yana umuhimu kwa wahifadhi wa lugha wanaoandaa nyenzo za Kibukusu. Uainishaji huu unatoa msingi wa kufundishia sentensi changamano. Umuhimu huu ni mkubwa hasa kwa vijana. Vijana hawa wanaishi katika mazingira yenye mwingiliano mkubwa wa Kiswahili na Kingereza

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Utafiti huu ulilenga kujibu swali: Kuna aina zipi za vishazi tegemezi katika sentensi za Kibukusu? Matokeo yanaonesha aina sita. Hizi ni kishazi kirejeshi, cha mahali, cha wakati, cha sababu, na cha masharti. Aina ya sita ni ya kipekee. Inaitwa kishazi cha utangulizi. Kinatumia viambishi *nekhanja* au *nekharakikha*. Fasihi iliyopo ya Kibantu haijawahi kukibainisha waziwazi. Fasihi ya jumla inatambua mfumo wa aina tatu za vishazi tegemezi. Matokeo haya yanapingana na mfumo huo. Vielezi vya Kibukusu havikai kama kundi moja. Badala yake, vinagawanyika katika aina nne. Nadharia ya X-Baa ilifaa kuchanganua aina zote sita. Kila aina ina kichwa chake cha kisintaksia. Kichwa hicho ndicho kinachosimamia muundo wake. Matokeo haya yana maana kubwa. Kwanza, yanathibitisha kuwa lugha ndogo za Kibantu zina utajiri wa kisintaksia. Hii ni kweli hata kwa lugha zisizo na fasihi kubwa ya kiisimu, kama Kibukusu. Utajiri huu unazidi matarajio ya nadharia zilizojengwa kutoka lugha chache zinazosomwa zaidi. Aidha, mbinu ya kimaelezo inayotumia data halisi za wazawa ina uwezo mkubwa. Inaweza kufichua miundo ambayo tafiti za awali za Kenya hazikuibaini. Kwa msingi huu, utafiti huu una michango mitatu. Mosi, unachangia data mpya za Kiafrika kwa nadharia za kimataifa za kisintaksia. Pili, unatoa msingi wa kuchunguza miundo ya kina na sheria za kisarufi za vishazi hivi. Msingi huu utafaa katika tafiti pana zaidi zijazo. Tatu, unaweka msingi wa kuhifadhi lugha ya Kibukusu.

Mapendekezo: Tafiti za baadaye zinapaswa kuchunguza kwa undani zaidi tofauti za kilahaja na kizazi zilizojitokeza katika data, hasa kuhusiana na viambishi vya wakati. Aidha, tafiti hizo zinapaswa kulinganisha kishazi cha utangulizi cha Kibukusu na lugha nyingine za Kiluhya na Kibantu za Afrika Mashariki ili kubaini ikiwa ni sifa ya pekee ya lahaja hii au sifa pana ya kikundi hiki cha lugha. Vilevile, matokeo haya yanaweza kutumika kama msingi wa kuandaa nyenzo za kufundishia Kibukusu na kuhifadhi lugha hii kabla ya kuathiriwa zaidi na mwingiliano wa lugha nyingine.

MAREJELEO

Aboh, E. O., & Essegbey, J. (2010). General properties of the clause. In E. O. Aboh & J. Essegbey (Eds.), *Topics in Kwa syntax* (pp. 39–64). Springer. https://doi.org/10.1007/978-90-481-3189-1_3

Agbo, M. S. (2023). A functional typology of Igbo multi-verb constructions. In J. Fleischhauer & C. P. Kihara (Eds.), *African languages from a Role and Reference Grammar perspective: Studies on the syntax-semantics-pragmatics interface* (pp. 25–50). düsseldorf university press. https://doi.org/10.1515/9783110795295-002

Asiimwe, A. (2019). The syntax of relative clause constructions in Runyankore-Rukiga: A typological perspective. *Stellenbosch Papers in Linguistics Plus, 58*, 131–154. https://doi.org/10.5842/58-0-840

Baligira, J. (2025). [Review of the book *History, identity and the Bukusu-Bagisu relations on the Kenya and Uganda border*, by P. W. Wekesa]. *African Studies Review, 68*(1), 201–202. https://doi.org/10.1017/asr.2024.164

Bans-Akutey, A., & Tiimub, B. M. (2021). Triangulation in research. *Academia Letters*, Article 3392. https://doi.org/10.20935/AL3392

Beermann, D. (2024). Akan focused questions and relative clauses in discourse: The role of the particle *na*. *Studies in African Linguistics, 53*(1–2), 166–189. https://doi.org/10.32473/sal.53.1and2.135192

Božić, L. (2022). *On the polysemy of connectives introducing subordinate clauses of cause in English and Croatian* [Bachelor's thesis, Josip Juraj Strossmayer University of Osijek]. FFOS Repository. https://repozitorij.ffos.hr/islandora/object/ffos:6132

Candrasius, Y. (2024). *An analysis of subordinate clauses in complex sentences found in the "Online CNN Newspaper"* [Master's thesis, Universitas Mahasaraswati Denpasar]. Universitas Mahasaraswati Denpasar Institutional Repository. https://eprints.unmas.ac.id/id/eprint/7746/

Carter, N., Bryant-Lukosius, D., DiCenso, A., Blythe, J., & Neville, A. J. (2014). The use of triangulation in qualitative research. *Oncology Nursing Forum, 41*(5), 545–547. https://doi.org/10.1188/14.ONF.545-547

Chomsky, N. (1986). *Knowledge of language: Its nature, origin, and use*. Praeger.

Chomsky, N. (2020). Remarks on nominalization: Background and motivation. In A. Alexiadou & H. Borer (Eds.), *Nominalization: 50 years on from Chomsky's Remarks* (pp. 25–28). Oxford University Press. https://doi.org/10.1093/oso/9780198865544.003.0002

Clarke, V., & Braun, V. (2014). Thematic analysis. In T. Teo (Ed.), *Encyclopedia of critical psychology* (pp. 1947–1952). Springer. https://doi.org/10.1007/978-1-4614-5583-7_311

Cowper, E. A. (1992). *A concise introduction to syntactic theory: The government-binding approach*. University of Chicago Press.

Downing, L. J., & Marten, L. (2019). Clausal morphosyntax and information structure. In M. Van de Velde, K. Bostoen, D. Nurse, & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (2nd ed., pp. 270–307). Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315755946-9

Haegeman, L. (1994). *Introduction to government and binding theory* (2nd ed.). Wiley-Blackwell.

Jeremiah, L. (2019). *Uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha Kisukuma: Mtazamo wa X-Baa* [Master's thesis, The Open University of Tanzania]. The Open University of Tanzania Repository. https://repository.out.ac.tz/3035/

Kaji, S. (2024). Homology of the object relative clause and the temporal subordinate clause: Considerations from Nyoro, a Bantu language of western Uganda. *Kyoto Sangyo University Essays. Humanities Series, 57*, 63–104. https://nrid.nii.ac.jp/nrid/1000010134751/

Kisembe, E. (2018). Verb raising and wh-movement in Bukusu. *Arusha Working Papers in African Linguistics, 1*(1), 24–37. https://arushalinguistics.org/publications/Kisembe_AWPAL_2018.pdf

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International.

Maddieson, I., & Sands, B. (2019). The sounds of the Bantu languages. In M. Van de Velde et al. (Eds.), *The Bantu languages* (pp. 79–127). Routledge.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbuki, K. (2019). *Clause chaining in Kisukuma: A role and reference grammar approach* [Master's thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Digital Repository. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/109690

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2003). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches* (2nd ed.). ACTS Press.

Mutonyi, N. (2000). *Aspects of Bukusu morphology and phonology* [Doctoral dissertation, The Ohio State University]. OhioLINK Electronic Theses and Dissertations Center. http://rave.ohiolink.edu/etdc/view?acc_num=osu1488203552780873

Mwamzandi, M. (2022). The pragmatics of Swahili relative clauses. In G. Sibanda, D. Ngonyani, J. Choti, & A. Biersteker (Eds.), *Descriptive and theoretical approaches to African linguistics: Selected papers from the 49th Annual Conference on African Linguistics* (pp. 227–246). Language Science Press. https://doi.org/10.5281/zenodo.6393758

Nyandago, F. O. (2013). *Uchanganuzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii* [Master's thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Digital Repository. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/60461

Paolillo, J. C., & Das, A. (2006). *Evaluating language statistics: The Ethnologue and beyond*. UNESCO Institute for Statistics.

Radford, A. (1997). *Syntax: A minimalist introduction*. Cambridge University Press.

Sikuku, J. M. (2011). *Syntactic patterns of anaphoric relations in Lubukusu: Representation and interpretation in a minimalist perspective* [Doctoral dissertation, University of Nairobi]. University of Nairobi Digital Repository. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/1541bbc5-0892-4f88-932b-36c5b06fdf86

Van de Velde et al. (Eds.), *The Bantu languages* (pp. 270–307). Routledge.

Van de Velde, M. (2019). Nominal morphology and syntax. In M. Van de Velde, K. Bostoen, D. Nurse, & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (2nd ed., pp. 237–269). Routledge.

VanderStoep, S. W., & Johnson, D. D. (2008). *Research methods for everyday life: Blending qualitative and quantitative approaches*. Jossey-Bass.

Vogel, A. (2022). *A typology of finite subordinate clauses in Jarawara*. Cadernos de Etnolingüística, Série Monografias 6.

Wakarindi, P. M. (2018). *Clause complexity in Gĩkũyũ: A functional account* [Doctoral dissertation, Kenyatta University]. Kenyatta University Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/ac2a25dc-baad-480a-99fb-bab374d61e6d

Watulo, A. W. (2020). Aspect marking in Kibukusu. *Bayan: A Journal of Language and Linguistic Studies, 1*(1), 10–19. https://www.researchgate.net/publication/358349016_Bayan_A_Journal_of_Language_and_Linguistic_Studies_A_Journal_of_Language_and_Linguistic_Studies_BJLLS_Under_a_Creative_Commons_Attribution_40_International_License_Aspect_Marking_in_Lubukusu